*Jiwe la kiroho la kujengea No.93*

# SIRI YA KUCHAGULIWA KIMBELE

*"Na ndani yake sisi nasi tulifanya urithi, huku tukichaguliwa tangu awali sawasawa na kusudi lake yeye, ambaye hufanya mapenzi yake.Nasi katika huyo tupate kuwa sifa ya utukufu wake,sisi tuliotangulia kumwekea kristo tumaini letu."* (Waefeso 1:11-12).

Na tumezungumza juu ya neno la *kuchaguliwa tangu zamani*, mnaona, hilo linawakwaza watu wengi sana. Ni Neno la Mungu. Yeye analitumia, "kwa kuwa tumechaguliwa tangu zamani kwa Neno la Mungu."(Waefeso 1:3-5) Na Unapochaguliwa tangu zamani, mbona, lazima litukie, kwa kuwa hivyo ndivyo ilivyo. Mungu alikuchagua kwa sababu alijua utakachofanya tangu mwanzo. [1]

Sasa, Kitabu cha waefeso, kwa mawazo yangu, ni moja kati ya vitabu vikuu mno vya agano jipya. Inatuacha ambako ukalvini (kuchaguliwa kabisa tangu zamani) hukimbia kwa mguu mmoja, uaminianizimu (Hakuna kuchaguliwa kimbele) hukimbi na huo mguu mwingine, lakini kitabu cha waefeso kinachukua hayo pamoja na kuliweka mahali kanisa.

Kutangulia kuchagua huangalia nyuma kwenye kutangulia kujua, nako kutangulia kujua huangalia kwenye mwisho wa safari. Msije mkasahau jambo hilo, ya kwamba kuteuliwa huangalia huku nyuma, hili hapa, "Nilikuwa gugu. Nilizaliwa katika dhambi, nikaumbika katika uovu, nikaja duniani nikisema uongo, nilizaliwa kati ya wenye dhambi. Baba na mama na jamaa yangu yote, wenye dhambi. Nilikuwa gugu. Lakini, mara, nikawa chembe ya ngano. Ilitukiaje?" Hiyo, hiyo ni nini? Kuteuliwa. Mungu, kabla ya kuwekwa misingi ya dunia, aliteua kwamba hilo gugu litakuwa chembe ya ngano. "Sasa najua kwamba mimi ni chembe ya ngano, kwa sababu nimeokolewa. Ninafanya hivyo vipi?" Naangalia nyuma na kuona kwamba Yeye aliikusudia, zamani za kale. Kwa kutangulia kujua Yeye aliona ya kwamba mimi ningempenda, kwa hivyo akafanya upatanisho kwa njia ya Mwanawe Mwenyewe(II Wakorintho 5:18-19), ili kwa njia Yake nipate kutoka kwenye gugu niwe chembe ya ngano. "Sasa, niko wapi sasa?" Nimeokolewa, natembea katika neema ya Mungu. "Kutangulia kuchagua huangalia wapi?" Kwenye mwisho wa safari. "Yeye atanipeleka wapi, na ninaelekea wapi?" Hilo limekupata. Haya basi. [2]

Tulipewa urithi vipi, kwa njia gani? Kuchaguliwa tangu awali. Kuchaguliwa tangu awali ni kujua tangu zamani. Mungu alijuaje kwamba angekuaminisha kuwa mhubiri? Kujua kwake tangu zamani. "Si kwa uweza wa yeye atakaye wala yeye apigaye mbio, Ni Mungu mwenye kurehemu."(Warumi 9:14-16) Hiyo ni kweli, kuchagua tangu awali. Yeye alijua kilichokuwa ndani yako. Alijua kilichokuwa ndani yako kabla hata hujaja duniani. Alijua kilichokuwa ndani yako kabla hapajakuweko na dunia ambamo ungeishi. Huyo ni Yeye. Huyo ni Mungu asiye na kikomo, yule asiye na kikomo. Sisi tuna kikomo, tunaweza tu kuwazia yaliyo na kikomo. [3]

Yeye alimpa mwanadamu uhuru wa kujichagulia, “Kama ukichukua *hii* utaishi, na kama ukichukua *ile* utakufa.”(Mwanzo 2:15-17) Na kila mtu anayekuja ulimwenguni yungali amewekwa katika hali ile ile. Mungu, kwa kujua Kwake tangu zamani, alijua ni nani angefanya hivi na ni nani hangefanya.

Swali liliulizwa jana na mwanatheolojia, ambaye amekuwa akihudhuria mikutano hii ama akisikiliza kanda, kasema, “Swali moja!” Akasema, “Basi Mungu yuko kila mahali? Kisha,” akasema, “Anaweza kuwa kila mahali?”

Nikasema, “Yeye hayuko kila mahali jinsi neno linavyozungumzia kuwa kila mahali. Yeye hawezi kuwa Aliye Hai na awe kila mahali. Kama Yeye yu kila mahali, mbona basi uombe upewe Roho Mtakatifu? Kama Yeye yuko kila mahali, Yeye amejaza kila mwanya, kona, ufa, kila chembechembe, uzi, kila kitu kingine kilichopo.” Nikasema, “Mbona alimtafuta Musa, kama Yeye yuko kila mahali, mwishoni? Mbona Yeye alikimbia huko na huko katika bustani ya Edeni, akilia, ‘Adamu, Adamu, uko wapi?’ kama Yeye yuko kila mahali?”(Mwanzo 3:8-10).

Yeye yuko kila mahali kwa sababu Yeye anajua yote. Anajua yote kwa sababu Yeye hana mwisho, na kutokuwa na mwisho kunamfanya Yeye awe kila mahali. Akiwa kila mahali, halafu, akiwa asiye na mwisho, ndipo, Yeye huketi katika Mbingu. Anakaa mahali fulani kwa sababu Yeye ni Aliye Hai.

Lakini, akiwa asiye na kikomo, basi anajua mambo yote. Akijua kila wakati mbu anapopepesa jicho lake. Jinsi kila nyuki, anakoenda kwenye sega kupata asali yake. Yeye anajua kila shomoro anayeketi mtini. Yeye anajua kila wazo lililo moyoni mwako, kwa kuwa hana mwisho na anajua yote(Zaburi 139:1-18). Hiyo ni kusema, Yeye si asiye na kikomo tu, mbali ni mjua yote, anajua kila kitu. Bali Yeye ni Aliye Hai, Mungu ni Aliye Hai, kutoka kwa Aliye Hai huyu hapa yakaanza kutokea.

Kwa hiyo sasa, Mungu huweka. Yeye tayari amejidhihirisha Mwenyewe, Yeye ni Mungu. Tayari amejidhihirisha Mwenyewe kama Mwokozi, mwanadamu alipotea Naye akamwokoa(Waefeso 2:8). Tayari amejidhihirisha kama Mponyaji (Isaya 53:4-5). Haidhuru watu wanasema Yeye ni nani; Naye ndivyo alivyo, hata hivyo, vile vile. Yeye ni Mponyaji, Yeye ni Mwokozi, yeye ni Mungu, Yeye ni wa Milele. Naye ana kusudi. Na kusudi Lake lilikuwa, hapo mwanzo, kufanya viumbe ambao wangempenda na kumwabudu.

Naye akawafanya viumbe, navyo hivyo viumbe vikaanguka. Kisha Mungu, kwa kutokuwa kwake na mwisho, aliangalia katika mlolongo wa wakati na kuona kila mtu ambaye angeokolewa. Kila mtu, alijua hayo kwa kujua tangu zamani. Kwa hiyo kama Yeye, kwa kujua Kwake tangu zamani, alijua nani angeokolewa na ni nani hangeokolewa, angeweza kuchagua tangu zamani (I Timotheo 2:3-4). Kwa hiyo, ili awashike wale ambao wangeokoka, ilimbidi kufanya upatanisho kwa ajili ya dhambi zao.(I Yohana 2:2)

Yeye alituchagua tangu zamani tupate Uzima wa Milele, akijua kwamba wale ambao wangeweka kando kila kitu, na hata ionekane ni gumu vipi kwa wana wa ulimwengu, haingemaanisha cho chote, kwa kuwa wao walikuwa wana wa Mungu.

Naye aliwaita (Matendo2:38-39), Naye akamtuma Yesu, kusudi Damu Yake iwe upatanisho, Upatanisho wa Damu, kufanya upatanisho, au kukubalika, au utakaso daima. Si wakati mmoja tu kwenye ufufuo, bali “yu hai sikuzote, akiwaombea,” (Waebrania 7:25), hivi kwamba Mkristo

anawekwa msafi mchana na usiku. Kuna Damu ya Yesu Kristo inayofanya kibali msalabani pale (Wakolosai 1:18-20), katika Uwepo wa Mungu, ambayo hutusafisha daima, mchana na usiku, na dhambi zote(Warumi8:33-34). Nasi tumeingizwa ndani salama(II Timotheo 2:19). Kuingizwa ndani vipi? Na Roho Mtakatifu, katika Mwili wa Bwana Yesu (I Wakorintho 12:13), na tuko salama. "Yeye ayasikiaye Maneno Yangu na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa Milele na hataingia hukumuni kamwe, bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani."(Yohana 5:24) Hakuna hukumu tena! Mkristo haingii hukumuni(Warumi 8:1). Kristo aliingia kule kwa ajili yake. Wakili wangu alisimama mahali pangu. Yeye alinitetea, ya kwamba sikujua. Yeye alimwambia Baba kwamba sikustahili, ya kwamba sikujua kitu. Bali alinipenda na akapachukua mahali pangu, na akanitetea, na leo niko huru! Naam, bwana. Naye aliimwaga Damu Yake, kuitoa pale kwa ajili ya dhambi zetu.( Waebrania 9:11-12; Warumi 5:8-10). [4]

Basi, Mwana-Kondoo, katika wakati wa upatanisho *hapa* nyuma, Yeye alijua ya kwamba kulikuwako na majina ndani humo yaliyowekwa ndani humo tangu kuwekwa misingi ya dunia (Ufunuo 17:8). Na mradi majina hayo hayajadhihirishwa duniani bado, ilimbidi Yeye kukaa hapo kama Mpatanishi. Mnaelewa? Kuchaguliwa tangu zamani, kikamilifu!.....

Vema. Ilimbidi kukaa pale, kwa sababu Yeye alikuja kuwafia wale ambao Mungu aliwakusudia Uzima wa Milele (Matendo 13:48). Kwa kujua Kwake tangu zamani, Yeye aliwaona. Si kwa mapenzi Yake Mwenyewe; mapenzi Yake yalikuwa kwamba hata mmoja asipotee. Lakini kwa kujua Kwake tangu zamani Yeye aliwajua wale ambao wangepotea na wale ambao hawangepotea(I timotheo 2:3-4).

Kwa hiyo, mradi tu kulikuwa na jina moja ambalo lilikuwa bado, kamwe halijatangazwa duniani, ilimbidi Kristo kukaa hapo kama Mpatanishi, kushughulikia jina hilo. [5]

Lakini Mungu alihitaji mauti, upatanisho(Warumi 6:23; Waebrania 2:9-10: Waebrania 9:22). Sasa, kuna tofauti kubwa sana kati ya dini na wokovu. Dini ni kifuniko. Wokovu ni Kuzaliwa, karama ya Mungu, wala hauwezi kupatwa na mtu ye yote wala kundi lo lote la mwanadamu. Mungu humletea mtu binafsi karama hii( Warumi 3:21-26). Na karama hizi za Uzima wa Milele zilikusudiwa na Mungu kwa ajili ya kila mtu binafsi kabla hata hatujakuwa na ulimwengu, kulingana na Maandiko. Biblia ilisema, katika Ufunuo, ya kwamba mpinga-Kristo aliyekuwa aje juu ya nchi, angewadanganya wote walioishi juu ya nchi, ambao majina yao hayakuandikwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu (Ufunuo 13:8). Mungu, kwa kujua Kwake tangu zamani, aliona ni nani angekuja na ni nani asingekuja, Kristo alishuka kufanya njia kwa ajili ya wale ambao wangekuja. Unaona, kuwajua hao wengine(Matendo 22:14).

Kama Yeye ni Mungu, kweli, hana budi awe hana kikomo. Na kama hana kikomo, Yeye hawezi kuwa hana kikomo bila kuwa mwenye nguvu zote. Hawezi kuwa mwenye nguvu zote bila kuwa yuko kila mahali. Hawezi kuwa anayeenea kila mahali bila kuwa mwenye kujua yote. Kwa hiyo, unaona, yote hayo yanamfanya Yeye kuwa Mungu.

Kwa hiyo, Yeye alijua mwisho tangu mwanzo. Yeye alijua ni nani atakuja na ni nani hatakuja, na alijua kutakuwako na wengi watakaokuja, kwa hiyo akamtuma Kristo kufanya upatanisho kwa ajili ya hao ambao wangekuja. Sasa, hakuna jambo tunaloweza kufanya lililo na

uhusiano wote na jambo hilo. Yesu alisema, “Wote alionipa Baba,” alionipa wakati uliopita, “watakuja Kwangu. Wala hakuna mtu anayeweza kuja asipovutwa na Baba.”( Mt Yohana 6:37,44; 10:27-30) Unaona? Sasa, unaona, yote yako katika kujua Kwake Mungu.

Unasema, “Ndugu Branham, je! mimi nimo ndani?” Sijui. Ninatumaini ya kwamba nimo. Tunatimiza wokovu wetu wenyewe kwa kuogopa na kutetemeka(Wafilipi 2:12-13).Sasa, Kanisa limechaguliwa kukutana na Mungu bila waa wala kunyanzi.(Waefeso 5:25-27). Sasa, kama tuko katika Kanisa Hilo, tumechanguliwa tangu awali kwenye Kanisa hilo. Sasa jichunguzeni kwa Neno, Ndipo mnapoweza kuangalia tuko umbali gani( II Wakorintho 13:5). [6]

Niliwaambia , Wokovu ni jambo la kibinafsi kati ya Mungu na mwanadamu peke yao: mtu mmoja, anatafuta wokuvu wetu kwa hofu na kutetemeka. Na sijui msingi mwingine, kama mwalimu, au kama mhudumu kutoka kwa Kristo, zaidi ya kuliweka hapojuu ya Neno.Siwezi kuliweka Mahali pengine popote. [7]

Mungu alijua mwisho tangu mwanzo, hivyo basi Yeye angeweza kupanga kila kitu, kwamba ingeweza tu kufanya kazi kwa utukufu Wake(Warumi8:28-30). Na hiyo inatupatia ujasiri, kujua kwamba haijalishi ni nini kinachotukia, Mungu anafanya kila kitu, saa inapiga tu kwenye wakati hasa (Waefeso 1:3-6).

Wakati mwingine tunakuwa wachovu, tumevurugika. Tunakuwa na pupa. Tunawazia, “Loo, lazima tufanye *hili*, au tufanye *lile*.”

Lakini, kumbuka, saa ya Mungu itakuwa tu kwenye wakati hasa. Mambo haya yote hayana budi kuwa hivi. Yote hayana budi kufanywa kulingana na maarifa Yake makuu, kujua Kwake kimbele, kwani kwa kujua kimbele Yeye aliweza kuchagua kimbele, si kwa shauku Yake, bali kwa kujua Kwake kimbele. Mungu hachagui kimbele kwa shauku Yake. Yeye hataki mtu yeyote aangamie, lakini kwa kujua Kwake kimbele Yeye alijua ni nani angelikubali na ni nani asingekubali. Hivyo basi Yeye anaweza kufanya kila kitu kifanye kazi kulingana na saa Yake kubwa inayopigapiga, kwa kuwa Yeye angeweza kutaja kimbele mwisho tangu mwanzo. Na, kwa hiyo, Yeye alijua kwamba sisi tungeishi katika siku hii. Alijua kwamba hii ingekuwa ni siku yetu. Alikuwa na mipango kwa ajili ya siku hii. Amekuwa na mipango kwa ajili ya kila siku. Na kamwe hata mpango Wake mmoja haujawahi kushindwa. Yeye daima huwa kwenye wakati ufaao(Mhubiri 3:1-11). [8]

Yeye hufunua Neno Lake tu kwa waliochaguliwa tangu zamani. Sasa, ninapotumia neno *kukusudiwa tangu zamani*. Sasa, ni neno baya la kutumia hadharani, hasa sana wakati tunapokuwa na makundi yaliyochanganyikana kati ya Waamenia na Wakalvini. Nimewaomba msifikirie mimi ni mjuvi, lakini wote wawili wamekosea kulingana na Maandiko. Neema ni yale Mungu aliyonitendea, kazi ni yale ninayomfanyia Yeye (Yakobo 2:14-26).

Lakini neno hilo, ninapolitumia, *kuchaguliwa tangu zamani*, hilo ndilo neno tu ninalojua jinsi ya kulifanya…Ni kujua kwa Mungu tangu zamani, unaona, kwamba Yeye alijua. Alikufa ili

wote wapate kuokolewa(Waebrania 2:9), alikufa, bali kwa kujua kwake tangu zamani Yeye alijua ni nani angeokolewa na ni nani asingeokolewa. Hayo ndiyo yale anayojua, mimi sijui wala wewe hujui, kwa hiyo tunatimiza wokovu wetu wenyewe kwa kuogopa na kutetemeka(Wafilipi2:12-13).

Sasa, lakini Mungu ameweka Neno Lake, na ameliweka katika nyakati zote. Kujua Kwake tangu zamani kumemfanya aweke kanisani, na katika watu, mambo fulani aliyofanya tangu mwanzo. Halafu Injili inayohubiriwa kwa wakati *huo* inafunuliwa tu kwa watu fulani, hao wengine hawalioni(Mathayo 13:10-17). "Nakushukuru, Baba, umeyaficha mambo haya machoni pa wenye hekima na elimu, ukawafunulia watoto wachanga wanaoweza kulifahamu." (Mathayo 11:25). Huko ni kuchaguliwa tangu zamani. Si kwamba alifanya jambo hilo kwa, unasema, "Nitakuchagua wewe, bali wewe sitakuchagua." Kwa kujua Kwake tangu zamani, Yeye alijua utakachofanya.

Sasa, Yeye hufunua mambo kwa kujua Kwake tangu zamani kwa hao ambao Yeye amewachagua kwa ajili ya mambo haya, la sivyo hawalioni. Wanasimama pale pale, wakiliangalia, wala hawawezi kuliona( Isaya 6:9-10). Kwa kujua kwa kimbele Yeye alichagua mambo haya kutokea(II Petro 1:21; II Timotheo 3:16-17).

Yeye hujichagulia mtu Wake mwenyewe kwa kujua Kwake tangu zamani. Kama alivyosema katika Warumi 9:10-13 hapa, ya kwamba kuchagua kwa Mungu kupate kusimama imara…. Ya kwamba Esau na Yakobo wote wawili walizaliwa na wazazi watakatifu, mapacha, ili kwamba kuteua Kwake kupate kusimama imara na kuwe ni kweli, Yeye alisema, "Ninamchukia Esau, na ninampenda Yakobo," kabla hata mmoja wa hao wavulana kuzaliwa. Unaona? Yeye anajua kilicho ndani ya mwanadamu, alijua tangu mwanzo ilikuwa ni kitu gani, kwa hiyo Yeye anaweza kufanya kila kitu kitende kazi kwa wakati wake kabisa. Sisi huwa na wasiwasi sana na kuhangaikahangaika; hujapata kumwona Yeye akihangaika, hawahangaiki. Unaona? Kila kitu kinatenda kazi sawasawa, barabara kabisa, saa inasonga mbele. [9]

Hiyo ndio njia pekee utayomjua yeye leo (Yohana 17:3), Njia pekee utakayopata ufunuo wa Utatu wa Mungu ni kwa Roho Mtakatifu. Na njia pekee inayowezakua, ni wewe ulichaguliwa tangu asili kuliona hili. Kama si hivyo, kamwe hutaliona. Ikiwa hukuchaguliwa kimbele kuliona, kamwe hutaliona; kwa sababu ile Nuru inaweza kumulika na ukaenda zako na kuidhihaki na kulielezea hilo huko, kwa mawazo ya kiakili. Wakati Mungu yule yule, Mwenyewe akijidhihirisha na kulithibithisha hilo, unaona? ila, ikiwa hukuwekewa kuliona, hutaweza kuliona.

Mungu hakuwahi kusema tu, "Nitamchagua huyu, nimchague Yule…" Sababu Aliweza kuchagua kimbele, kwa kuwa Yeye hana Kikomo, Yeye hujua kila kitu. Yeye hana kikomo, hivyo, kwa hiyo Yeye alijua kila kitu. Alijua mwisho. na aliweza kusema mwisho tangu mwanzo.Yeye ni Mungu. Ikiwa hawezi kufanya hivyo, Yeye si Mungu. Ndiyo bwana. Yeye hana kikomo. [10]

Ninaamini kuna Bibi-arusi aliyechaguliwa tangu zamani. Ninaamini Mungu alisema Yeye angekuwa na Kanisa lisilo na waa wala kunyazi(Waefeso 5:25-27). Ninaamini katika kuchaguliwa tangu zamani: ya kwamba Bibi-arusi amechaguliwa tangu zamani (Waefeso 1:3-9);

Yeye hana budi kuwepo pale. Ninatumaini niko pamoja Naye. Niko pamoja Naye. Sasa, ni juu yangu kutimiza wokovu wangu na Mungu mpaka mambo haya yamekubaliwa na Mungu halafu yakatiwa muhuri katika Ufalme wa Mungu. Huyo hapo Roho Mtakatifu. Hizo hapo kazi halisi za Mungu. Imetiwa muhuri hata siku ya ukombozi (Waefeso 4:30).

Hebu niliseme vizuri sana kusudi mlipate: Kanisa limechaguliwa tangu zamani kuwepo. Nataka kuwa pamoja Nalo, bali njia pekee nitakayokuwa pamoja Nalo, ni kuwa sehemu Yake.

Ninakuwaje sehemu Yake? Kwa kuwa ndani Yake. Ninaingiaje ndani Yake? Kwa ubatizo, kwa Roho mmoja. I Wakorintho 12:13, "Kwa Roho Mmoja sote tumebatizwa kuwa Mwili mmoja…nasi sote tumenyweshwa Roho mmoja" Mwili mmoja, tumebatizwa ndani Yake (IWakorintho 12:27).

Bali huwezi kuvishikamanisha vitu hivi vidogo, useme, "Nilinena kwa lugha. Nimempata Huyo." Unatoka unaenda hapa nje, nawe una hasira, na unaapa, na kufanya yasiyofaa , huko ni kutia manyoya ya tausi kwenye ndege mwenye milio. Mnaona? Huwezi kufanya jambo hilo. Maisha yako mwenyewe yanathibitisha ya kwamba sivyo ilivyo. Bali wakati vitu hivi vinafanya kazi ndani yako kwa njia ya Mungu, basi umetiwa muhuri (Waefeso 1:13-14). Ndipo basi hakuna kuiga kuhusu hilo. Wewe ni wewe tu. Hapo ndipo maono, kazi kamilifu za Roho Mtakatifu wa Mungu, kila kitu kinadhihirishwa. Kwa sababu gani? Wewe na Kristo mnakuwa mmoja (natumaini jambo hilo linaeleweka), wewe na Kristo mnakuwa mmoja (Waefeso 4:4-6).[11]

Mungu, Kabla ya misingi ya ulimwengu, Ambaye alijua mwisho tokea mwanzoni, kwa kujua kimbele Yeye alichagua pa kuishia; Alijua tofauti kati ya Yakobo na Esau.Yeye alijua tofauti kati ya mdhambi na Mtakatifu.Alijua tofauti. Alijua shauku ya kila moyo, hivyo alituchagua tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu na kuweka majina yetu katika kitabu cha Uzima cha mwanakondoo; na pia Mwanakondoo aliyepaswa kuchinjwa ( na kuweka majina yetu kabla hajachinjwa), na Biblia inasema Kristo alikua Mwanakondoo aliyechinjwa kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Alipochaguliwa nyuma pale kuwa Mwanakondoo kwaajili ya kuchinjwa, tulichaguliwa kua miongoni mwa ambao amechinjwa kwaajili yao (Ufunuo 13:8). [12]

Basi, wakati Mungu alipomchinja Mwana-Kondoo, katika mawazo Yake Mwenyewe, kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, kuthibitisha sifa Zake, alichokuwa Yeye; wakati Mwana-Kondoo alipochinjwa, tulichinjwa pamoja Naye. Wakati Damu ya Mwana-Kondoo iliposhikwa katika nia Yake Mwenyewe, kule nyuma kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, jina langu na majina yenu yaliandikwa kwenye kile Kitabu wakati huo, yote katika mawazo Yake makuu. Yeye hana kikomo. Kama sivyo alivyo, kwa nini akaruhusu jambo hilo? [13]

Wakati mwingi tunapoyatazama Maandiko kwa njia yetu wenyewe ya kuyatazama inaonekana gumu sana, bali tukisoma kwa bidii punde tu, tutaona ya kwamba Mungu mwenye hekima yote anajua kile hasa anachofanya. Naye anajua jinsi ya kufanya mambo haya na jinsi ya kumshughulikia mwanadamu. Anajua yaliyo ndani ya mwanadamu (IWakorintho 2:11-16).

Anamjua. Hatujui. Tunajua tu kwa akili zetu. Yeye anajua kilicho katika mwanadamu.Kwa kuwa Bwana hutafutatafuta mioyo yote ya fikira (I Nyakati 28:9)

Tunaona Musa vile alizaliwa ulimwenguni kijana mwanamume aliye na kipawa. Alizaliwa nabii, mkombozi. Alizaliwa na vifaa hivyo ndani yake alipozaliwa, kama vile kila mtu ajaye ulimwenguni huzaliwa na vifaa hivi. Kama ninavyoamini kabisa katika kujua kwa Mungu tangu awali, kule kuchaguliwa tangu awali—si eti kwamba Mungu anapenda mtu ye yote apotee, bali wote wafikie toba—bali akiwa Mungu, ilimpasa kujua, naye ajua mwisho tangu mwanzo. Kama hajui, basi Yeye si ye asiye na kikomo; na kama Yeye si asiye na kikomo, Yeye si Mungu. Kwa hivyo hakupenda, bila shaka, mtu ye yote apotee, bali Yeye, akijua ni nani atakayepotea, na ni nani hangepotea.

Hiyo ndiyo sababu,kusudi halisi la kuja kwa Yesu duniani kulikuwa kuwaokoa wale Mungu kwa kujua Kwake tangu awali aliwaona na akataka waokolewe, kwa sababu ulimwengu wote ulikuwa umehukumiwa. Sioni jinsi tungalifundisha hayo kwa njia nyingine ye yote ila kujua kwa Mungu tangu awali, na Biblia inasema dhahiri kwamba Yeye ajua mwisho tangu mwanzo na anaweza kuinena. Kwa hivyo, watu wanapojaribu kujifanya kitu wasicho, wanafanya muigizo tu, na hakuna budi watatambulikana. Dhambi zako hukupata. Huwezi kuzifunika. Kuna kifuniko kimoja cha dhambi. Hiyo ni Damu ya Bwana Yesu Kristo, na haiwezi kutumiwa isipokuwa Mungu alikuita tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu.[14]

Oh, natumaini Mungu ameliweka hili mioyoni mwenu. Sio chochote ungeweza kujielimisha kwacho, sio kile ungesoma ndani yake. Ni kile Mungu, Kwa uchaguzi, amefanya kwaajili yako. “si katika uwezo wa Yule atakaye, wala yule apigaye mbio; bali wa Yule arehemuye, yaani Mungu” (Warumi 9:14-16). [15]

Daima ninawashurutisha watu, “Nendeni kanisani, haidhuru mnaenda wapi.” Nami nimewaona watu kwa namna fulani wakirudi nyuma, na wakienda namna *hii*. Ndipo nikawazia, “Kuna nini?”Nikawaendea baadhi yao, “Siku ya kwanza ukiwa hapo, watakujia, ‘Jiunge na kanisa letu.’ Usipojiunga, hukaribishwi.” Ni jambo la kulazimishwa, unalazimishwa nalo, na hiyo ni Babeli. Lakini katika Kristo, unaingia kwa kuteuliwa; sio kwa kulazimishwa, moyo wako unakuvuta ndani. [16]

Mengi ya maswali haya hapa juu ya (Bibi arusi na Kanisa): “Vema, je, Bibi-arusi ata…” “Je, *hili* lita-…?” “Kanisa na…” Ona? Huwezi kutenganisha yalivyo. Bibi-arusi ni Mteule wa Mungu (Yohana 15:16). Kanisa litapiti (Dhiki).Hao ndio wale Hilo linasema, “Yeye atakaye, na aje.” (Ufunuo 22:17). Lakini Bibi-arusi ni Mteule wa Mungu.

Kuna huduma tano zilizoteuliwa na Mungu. “Kwa kuwa Mungu ametoa Kanisani mitume, manabii, waalimu, wachungaji, wainjilisti.” (Waefeso 4:11; I Wakorintho 12:28-30). Mungu alifanya hilo. Mwanadamu ana mashemasi na wengineo, na kadhalika, lakini mwaona, bali Mungu aliwaweka Kanisani kwa kusudi la kukamilisha Kanisa--huwezi kuligawanya. [17]

Kuna wengi wa wanaojifanyakuamini wakiendelea kusisimka na mambo tofauti kama hayo. Lakini wakati unapoamini hilo moyoni mwako ( Warumi 10:8-10), Wakati jambo Fulani limetokea kwako, ni Mungu aliyefanya hilo, na Mungu ndiyo pekeeanayweza kulifanya hilo. Kwahiyo Mungu kwa Neema na uchaguzi ameliweka hilo moyoni mwako uliamini hilo. Halikua hapo kwa kuanzia, na wewe Hauna njia ya kuliweka hapo. Mungu aliliweka hilo hapo na wewe ukaitikia mwito huo. [18]

Na ndipo wakati Roho Mtakatifu alipokuja…. nawe uko duniani, ukitembea hapa kama mwenye dhambi, ndani kabisa maishani mwako kuna kitu fulani. Hujui kinachotendeka, bali una njaa (Mathayo 5:6). Kuna kitu fulani ndani yako, kitu fulani ambacho hukukiweka humo ndani. Ni kitu fulani ambacho hungeweza kutamani kiwe humo ndani. Ni kitu ambacho ni kinyume na tabia asilia yako mwenyewe. Ni kujua kwa Mungu tangu zamani, kukitukia, Neno la Mungu. [19]

Roho Mtakatifu alitolewa ili apate kuleta Uhai kwa hizo Mbegu ambazo Mungu, kwa kujua Kwake tangu zamani, alijua kwamba zingekuwa hapa duniani. Kama alivyojua mbegu ya kwanza ya asili, Yeye anajua ambapo Mbegu ya Kiroho ipo. Mwili wako ulikuwa upo hapa wakati uo huo duniani, wakati Mungu alipoumba nchi mara ya kwanza. Sisi ni sehemu ya nchi. Tulikuwa tuko humo. Na kwa kujua Kwake tangu zamani Yeye alijua ni nani hasa angempenda na ni nani angemtumikia, na ni nani asingemtumikia. Kujua Kwake tangu zamani kunaonyesha jambo hilo. Kama hakuonyeshi, basi Yeye si Mungu. Hawezi kuwa Mungu bila kuwa hana kikomo. Na kama hana kikomo, Yeye anajua mambo yote. [20]

<u>Nukuu:</u>

[1] “Nguvu ya kugeuzwa” (65-1031M) Aya 237

[2] “Kufanywa wana wenye mamlaka I” (60-0515) Aya 106

[3] “Kufanywa wana wenye mamlaka IV” (60-0522E) Aya 89

[4] “Kufanywa wana wenye mamlaka III” (60-0522M) Aya 47-55

[5] “Muhuri wa kwanza” (63-0318) Aya 59

[6] “Kwanini ninayapinga madhehebu” (62-1111) aya 34-37

[7] “Lile shitaka” (63-0707) Aya 106

[8] “ Ishara kuu” (63-1129) Aya 10-12

[9] “ Kujaribu kumtumikia Mungu bila mapenzi yake” (65-1127B) Aya 131-139

[10] “ Kristo ni siri ya Mungu iliyofunulia” (63-0728) Aya 335-336

[11] “ Majina ya makufuru” (62-1104) Aya 172-175

[12] “ Wanawali kumi” (60-1211M) Aya 191

[13] “ Uzao wa Nyoka” (58-0928E) Aya 96-97

[14] “ Mbona unalia? Nena” (63-0714M) Aya 31-32

[15] “ Kusikia,Kutambua na kutendea kazi Neno la Mugu” (60-0221) Aya 57

[16] “Mahali pekee alipoandaa Mungu pa kuabudia” (65-1128M) Aya 204-205

[17] “ Maswali na Majibu” (64-0823E) COD, uk1005, Aya 53-54

[18] “Ibrahimu na Uzao wake baada unaomfuata” (61-0423) Aya E-33

[19] “ Muhuri wa Pasaka”(65-0410) Aya 63

[20] “ Mmoja katika milionioni moja” (65-0424) Aya 62-63

---

Jiwe la kiroho la kujengea na. 10 kutoka kwenye Neno lililofunuliwa la saa hii, Yamekusanywa na Gerd Rodewald friedenstr. 69 D-75328 Schomberg, Germany Simu (+49) 72357613 Fax: (+49) 72353306

---

Anakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia na kazi ya haraka itazunguka dunia. Na mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyokusudiwa kimbele imesikia.

(Ndugu Branham katika mwenendo utaratibu na mafundisho uk 724)

*Kwa nakala zaidi za kiingereza au kiswahili Andika kwa:*

*Joseph C Kanju*<br>
*Box 553 Korogwe - Tanga*<br>
*E-mail: kanjujoseph23@gmail.com*<br>
*Cellphone: 0654335361*